IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 4

Novemba 2021

# HabariNjema

KILA SIKU

**BURE**
HAKIUZWI
KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]

Uebert & BeBe
ANGEL


GoodNews
Become a
GoodNewsWorld
PARTNER
Your MiracleTV
GOODNEWS
IS EXPANDING
YOU CAN NOW WATCH
PROPHET UEBERT ANGEL 24/7 ON
PARTNER NOW AND HELP SPREAD
THE GOODNEWS AROUND THE WORLD
VISIT www.goodnewsworld.com/ partner




## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma ya Mungu, Uebert na Bebe Angel ni mapainia na sauti zinazoongoza kwenye kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion) pamoja na unabii duniani kote.Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu kama Habari Njema, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kwenye mikutano sehemu mbalimbali duniani, ni viongozi wa kidunia. Wanatambulika na kuheshimika kwa maono yao, uvumbuzi na ujasiri wao. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni kupitia mapenzi yao ya kuvuna nafsi na kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion).



**Kumbukumbu la Torati 32:10**
**"Alimkuta katika nchi ya ukame, Na katika jangwa tupu litishalo; Alimzunguka, akamtunza; Akamhifadhi kama mboni ya jicho;"**

Mungu ndiye Mpenzi halisi, na anatamani kuwa mwandani na wewe. Unapoelewa haya, unapoangalia Neno Lake, utagundua kuwa ni barua ya Mungu ya mapenzi kwako. Hutumia maneno kama andiko letu la leo kuelezea na kuwasiliana na wewe undani wa upendo wake kwako. Wewe ni "mboni ya jicho Lake, " ambayo ni nahau ya Kiebrania ambayo inaweza kutafsiriwa kama "mtu mdogo ninayemtazma daima." Hujapuuzwa; unaonekana. Mungu, ambaye anakaa Mbinguni na Dunia kama kiti cha miguu yake, macho yake daima yanakutazama. Haleluya! Biblia inasema kwamba macho ya Bwana ni safi sana hata hayawezi kuona chochote kibaya. Hiyo inamaanisha jinsi anavyokuona, haoni chochote kibaya juu yako. Anaona tu yaliyo sawa na mazuri kukuhusu. Anaiona haki yake mwenyewe ndani yako. Wewe ndiye akupendaye na anapendezwa nawe zaidi ya yote. Wewe ndiye picha anayoiona ikiakisi katikati ya macho yake. Na kama mpenzi wa kweli, Yeye pia anataka kuwa picha au mboni ya macho yako. Anataka kujiona anajidhihirisha katika macho yako. Lakini jinsi gani unamtazama kwa upendo Mungu asiyeonekana? Unafanya hivyo kwa kuangalia katika Neno Lake. Unapokazia macho katika Neno lake, unaona picha nzuri ya mwandani wako mpenzi.

## UKIRI WA KINABII

**Nimehifadhiwa, nalindwa, na kutunzwa na Mungu. Mtu yeyote anayenigusa, anagusa mboni ya jicho la Mungu. Anaponiangalia, Anaona kila kitu ambacho ni chema na safi na kizuri juu yangu. Ninapendwa sana na kufurahiwa naye zaidi ya yote.**

**SOMO LA ZIADA**
Habakuki 1:13; 2 Wakorintho 5:21



**Ufunuo 12:11**
**"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao......"**

Kuna sheria katika fizikia ambayo inasema kwa kila tendo, kuna mwitikio sawa na mwitikio kinyume. Walakini, kuna sheria ambayo ni bora kuliko sheria za fizikia au sheria nyingine yoyote ya asili. Ni sheria ya imani. Sheria hiyo inasema kwamba kuna hatua unaweza kuchukua katika mwili wa asili - nguvu ambayo unaweza kuitumia - ambayo itasababisha muitikio mkubwa rohoni. Imani hufanya yawezekane. Unapoamini kile Neno la Mungu linasema kuhusu wewe, kuna tendo sambamba unaweza kufanya katika mwili ambalo litalazimisha ulimwengu wa roho kukupa miujiza wako.Biblia inatuambia kwamba tunashinda kwa neno la ushuhuda wetu. Wakristo wengi wamekosa ufunuo katika hii. Wanaelewa aya hiyo kumaanisha kwamba unashuhudia baada ya kushinda ugumu huo au changamoto ambayo unakabiliwa nayo. Lakini sio hivyo inavyosema. Inasema kwamba unashinda kwa neno la ushuhuda wako. Unaona, imani sio kiitikio. Ni kitendaji. Ni nguvu ambayo, inapotumika, inashinda kila kikwazo. Hiyo inamaanisha sio lazima usubiri hadi maumivu yatoke ili kushuhudia uponyaji wako. Huna haja ya kusubiri hadi uone mamilioni kwenye akaunti ya benki ndipo ujitangaze kuwa tajiri. Unaweza kushuhudia makazi yako ya kudumu katika nchi unayochagua hata kabla ya kuona visa yako. Tumia sheria ya imani na ulazimishe miujiza yako idhihirike kwa neno la ushuhuda wako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamuru na ninatangaza kwamba muujiza wangu uko kinywani mwangu. Kwa imani, ninaingia katika maisha yangu ya baadaye na kudai kila baraka iliyo na jina langu. Mafanikio ni yangu. Utajiri ni wangu. Uponyaji ni wangu. Amani ni yangu. Ushindi ni wangu sasa hivi, katika Jina wenye nguvu wa Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 9:23; Warumi 10: 8



**Mathayo 6:34**
**"Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake…"**

Wewe sio wa kawaida. Kwa kweli, hakuna kitu cha kawaida juu yako. Watu wa kawaida wameajiriwa kufanya kazi kila siku. Siku zako, hata hivyo, zimeajiriwa kukufanyia kazi wewe. Watu wa kawaida wanalala usiku wakiwa na wasiwasi juu ya nini kitatokea kesho. Wanaamka asubuhi wakiwa na wasiwasi juu ya nini kitatokea kwenye siku hiyo. Lakini hayo sio maisha kwako. Andiko la leo linakuambia kuwa kesho yako imeajiriwa na Mungu kukusumbukia wewe kwa yote. Hiyo inaibakisha leo tu, na leo pia inapaswa kupewa majukumu yake. Imeumbwa na Mungu kuwa chombo cha furaha yako. Biblia inatuambia kwamba hii ndiyo siku ambayo Bwana ameifanya. Wajibu wako ni kushangilia na kufurahi ndani yake. Siku hii ya leo ipo ili kutoa nafasi katika muda kwa wewe kufurahia. Hakuna hata sekunde moja ya leo iliyotengwa kwa ajili ya wasiwasi, hofu, au mashaka. Unapoangalia saa, usione tena kama dakika zinazozidi siku yako. Badala yake, ikabili kila siku ukijua kuwa una sekunde 86,400 za kuiishia furaha na kuvinjari.

## UKIRI WA KINABII

**Mungu ameumba siku hii kama chombo cha kuibebea furaha yangu. Sitapoteza wakati wake kwa mawazo ya kuhofu au wasiwasi. Wasiwasi uko mbali nami, na sitakuja kuufikia na kuupata. Ninaishi maisha ya kutarajia furaha. Ninachagua furaha sasa na kila sekunde ya siku hii.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 118: 24; Wafilipi 4: 4



**Mwanzo 1: 2-3**
**"Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema, Iwe …"**

Biblia inatuambia kwamba hapo mwanzo, Roho wa Mungu alitulia juu ya uso wa vilindi. Neno hilo alitulia linamaanisha kupepesa daima katika mawazo bunifu yenye matokeo. Umepewa nguvu zilezile za kimungu. Wewe pia una uwezo wa kupepesa daima katika mawazo bunifu yenye matokeo. Kupepesa kwako kunaonekana kama kunong'ona. Hicho ndicho tafakari ya kweli inachofanya. Unaona, kile Roho Mtakatifu alikuwa akifanya ni kutafakari. Alikuwa akifikiria kwa kina juu ya matokeo anayoyataka. Kupitia kitengo cha mawazo na fikra, Aliviunda kama picha iliyokuwepo katika akili yake. Kisha akatangaza vitu alivyoviona na kuvifanya viwepo. Kama Wakristo, tuna njia bora ya kutafakari. Hatutoi kila kitu ili akili zetu ziwe tupu wakati tunatafakari kama watu wa ulimwengu wanavyofanya. Badala yake, tunajaza akili zetu na Neno la Mungu linalohusu kesho yetu au matokeo tunayotaka kuyaumba. Kisha tunanong'ona, tukijiongelesha wenyewe – uso wa kilindi - vitu tunavyotaka kuviona, kuvifanya, na tunavyotaka kuwa. Akili yako ni bodi ya maono ya maisha yako ya baadaye. Haijalishi unavyotamani ni vitu vinavyoonekana kuwa vya ajabu kiasi gan, ikiwa unaweza kuvifikiria, unaweza kuvipata. Piga picha ya maisha yako ya baadaye ukitumia lensi ya Neno. Viunde kwenye akili yako kwa kutumia mawazo ya fikra zako. Kisha vitamke kuvifanya vitokee.

## UKIRI WA KINABII

**Nimejaliwa uwezo wa kiungu wa kuiona kesho ninayotamani, kuiunda katika fikraz angu za kinabii, na kuiamuru iwepo. Ikiwa ninaweza kukidaka akilini mwangu, ninaweza kuiumba maishani mwangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yoshua 1: 8; Waefeso 3:20



**Luka 8:35**
**"Watu wakatoka kwenda kuliona lililotokea, wakamwendea Yesu, wakamwona mtu yule aliyetokwa na pepo ameketi miguuni pa Yesu, amevaa nguo, ana akili zake; wakaogopa...."**

Je! Unajua kwamba kila shirika bora la ndege ulimwenguni hubeba chumvi kwenye ndege zake? Ikiwa umewahi kusafiri kwa ndege, umeiona, lakini labda haujatambua kile unachokuwa ukiona. Ukiwa na tiketi ya daraja la Economy, unapopanda ndege, unapitia eneo fulani ambapo ni wachache tu waliochaguliwa wanaruhusiwa. Hapa panaitwa darasa la kwanza. Katika eneo hilo, kila kitu kinaonekana tofauti. Vitambaa na mpangilio wa viti ni wa hali ya juu kuliko ule wa daraja la Economy. Vifaa na vidokezo vimebuniwa kwa kuzingatia mahali pa mtu wa hadhi ya juu. Daraja la kwanza limeundwa maalumu kwa ajili ya mtu aliye na hadhi na ladha fulani. Mtu huyo ni wewe. Kila wakati tunasema kwamba Kanisa la Habari Njema Spirit Embassy ni kanisa la viwango. Kuna kitu juu yetu ambacho kinatuweka tofauti na wengine, ufunuo fulani ambao tumeelewa, ambao yule mwenye pepo katika andiko letu la leo pia alielewa. Kabla ya kukutana na Yesu, mtu huyu alikuwa akizunguka-zunguka akionekana mchafu. Jinsi alivyojibeba ilionyesha hali yake ya kiroho. Lakini baada ya kukombolewa, alifanyika chumvi. Na jambo la kwanza lililobadilika kwake ni mtindo wake, jinsi alivyovaa. Unapokutana na Yesu, lazima kuwe na mabadiliko yanayoonekana. Jinsi unavyoonekana kwa nje inapaswa kuonyesha mabadiliko yaliyotokea ndani. Wewe sio mtu wa "daraja la Economy" tena. Wewe ni daraja la kwanza, watu ambao wengine huwapita na kuwatamania.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yanaboreshwa dakika hii. Macho yangu yamefunguliwa kuona hadhi ya maisha inayonifaa mimi kama mtoto wa Mungu. Naishi ubora bila kuathiri uratibu wa fedha zangu. Mimi ni chumvi. Hakuna kitu kisicho na ladha kwenye maisha yangu. Mimi ndiye ladha, na mtindo wangu unabadilika sasa.**

**SOMO LA ZIADA:** Mathayo 5:13



**Mathayo 18: 2-4**
**"Yesu akamwita mtoto mdogo na kumsimamisha katikati yao. Naye akasema: "Amin, nawaambia, msipookoka na kuwa kama watoto wadogo, kamwe hamtaingia katika Ufalme wa Mbinguni. Kwa hiyo mtu yeyote anyenyekeaye kama huyu mtoto, ndiye aliye mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni." (NEN)**

Una uwezo wa kuwa tajiri au tajiri kuzidi Mark Zuckerberg. Haihitaji kueleke upande mwingine mpya wa uchakalikaji au kufanya kazi masaa mengi zaidi. Una rasilimali zote unazozihitaji sasa ili kuwa tajiri. Ni nguvu kubwa ya ajabu unayoimiliki, kwa watu wengi, haitumiki sana. Walakini, ni neema uliyopewa na Mungu ambayo inapatikana kwako kuitumia kama fursa. Hazina hii ya Ufalme ni alama ya umiliki inayoonekana ya kila Mkristo. Kiukweli, haiwezekani kujazwa na Roho na usiwe tajiri kwa namna hii. Je! Ni nguvu gani hii ya ajabu inayoweza kukufanya utajirika kuliko Mark Zuckerberg kila siku moja ya maisha yako? Ni tabasamu. Je! Unajua kuwa watoto hutabasamu Zaidi ya kama mara mia nne kwa siku? Haiwezekani kuwa karibu na mtoto anayetabasamu na usijazwe na furaha. Utafiti uligundua kuwa ni ngumu sana kukunja uso wakati wa kumtazama mtu anayetabasamu. Kutabasamu kunaambukiza. Kutabasamu ni kichocheo chenye nguvu kwenye kitovu cha raha cha ubongo wako kiasi kwamba hata ukiwa na tabasamu bandia, ubongo huachilia homoni za kujisikia vizuri mwilini kote ambazo zinakusaidia kujisikia vyema. Chokoleti, inayojulikana kuwa kiachilia raha bora, haiwezi kufikia nguvu ya tabasamu lako. Watafiti wa Uingereza waligundua kuwa tabasamu moja linaweza kutoa kichocheo kwenye ubongo kwa kiwango sawa na hadi chokoleti 2000. Utafiti huo huo uligundua kuwa kutabasamu linaleta msisimko wa raha sawa na mtu kupokea hadi Pauni 16,000 fedha taslimu. Hiyo ni karibu dolaa elfu 25. Kuwa kama mtoto mdogo na kuimarisha maisha yako kila siku kwa tabasamu.

## UKIRI WA KINABII

**Roho wa Mungu ndani yangu hutaijirisha roho yangu kwa furaha, huhuwisha nafsi yangu, na kuujaza mwili wangu wa nyama kwa nguvu. Tabasamu langu ni uthibitisho wa ukuu wangu. Tabasamu langu ni kibebeo cha habari njema. Ninapotabasamu, naachilia furaha ya Bwana na kuambukiza mazingira yangu na uwepo wake. Mfumo wangu wa kinga ya mwili unaongezewa uwezo zaidi, ulinzi wangu ni unaimarishwa maradufu, na ninamchanganya shetani.**

**SOMO LA ZIADA:** Isaya 12: 3; Wagalatia 5: 22-23



**Yohana 15:15**
**“Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu...**

Inawezekana kuwa rafiki wa Mungu. Sio tu inawezekana, lakini pia ni haki ya kipekee uliyopewa wewe kama mtoto wa Mungu. Mstari huu unatupa ufunguo wenye nguvu wa kuelewa siri ya urafiki na Mungu, na tumepewa na Mungu mwenyewe kupitia nafsi ya Yesu. Anawaambia wafuasi Wake, “nimewaita ninyi rafiki, kwa maana nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa Baba yangu” Mungu anasema wewe ni rafiki yangu kwa sababu nakujulisha Neno langu. Je! Unaona jinsi ilivyo rahisi kuitwa rafiki wa Mungu? Rafiki yake ni yule ambaye yuko tayari kusikia anachosema, yule ambaye Anashiriki naye siri Zake. Kanisa kwa ukubwa wake limepata ufunuo kwamba Mungu ni upendo (agape). Lazima pia tuelewe kwamba kutoka kwenye upendo wake wa agape, humimina upendo wake wa kirafiki (phileo) mioyoni mwetu. Anaonyesha hisia za mapenzi yake kwako kwa kushiriki Neno Lake nawe. Na unapozingatia Neno la Mungu, unaonyesha utayari wako kuwa rafiki Yake na kupokea mapenzi Yake. Unavutiwa na kile kinachomvutia, na kinachomvutia Mungu kuliko chochote ni kuona Neno lake linasikika na kuaminika. Hata wakati unasoma hii Habari Njema leo, unakuwa rafiki wa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana hupata pumziko ndani yangu. Mimi ni rafiki Yake wa kuaminika ambaye humfunulia siri Zake. Ninapokea mguso wa mapenzi Yake kwa kupokea Neno Lake kwa furaha. Daima niko tayari kusikia chochote Anachotaka kunishirikisha. Mimi ni bestie wa Mungu.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4: 8; Warumi 5: 5; 1 Wakorintho 2:10



**Wafilipi 1: 7**
**"Vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii..."**

Kuna njia mbili ambazo unaweza kufanikiwa katika maisha haya: unaweza kupambana kufika juu, au unaweza kuanzia juu. Kila mtu aliyekutangulia kwa kiwango kikubwa cha mafanikio ana makovu ya kudhibitisha. Watakuambia juu ya mapambano yao na kufeli kwao. Watazungumza juu ya makosa yao na kukatishwa tamaa kwao. Mafanikio yao ilikuwa safari kupanda mlima, na ingawa wao hatimaye walifanikiwa, ilikuwa ushindi mgumu wa kuupigania. Unaweza kuchagua kwenda hivyo, lakini kuna njia bora zaidi. Ulezi ni sampuli kifani iliothibitishwa. Yesu alitumia mfano wa ulezi alipowaita wanafunzi kumi na wawili, halikadhalika wewe na mimi, kufuata njia ambayo ameweka. Mlezi ni njia ya mkato ya mafanikio yako. Ukiwa pamoja na mlezi katika maisha yako, sio lazima uanzie chini. Dari yao inakuwa sakafu yako. Unapata faida ya mafanikio yao bila shida yoyote. Hivi ndivyo Mtume Paulo anachokimaanisha anaposema kuwa "washiriki wa neema yangu." Leo, neema imeachiliwa kwako kumtambua mtu huyo aliyewekwa ambaye unauishi ufunuo wake, mtu huyo ambaye amefanikiwa kiwango hicho cha mafanikio unachotamani ambaye neema yake itakuwa kombeo la kukurushia kileleni!

## UKIRI WA KINABI

**Neema ya kasi ya kiungu imeamshwa katika maisha yangu. Kinachochukua wengine miaka au miezi kukamilisha, mimi hufanikiwa katika muda mfupi sana. Macho yangu yako wazi kuona wasaidizi wangu, na ninatembea katika njia iliyoandaliwa. Sitakwepa maagizo au kukosa kumuheshimu yule aliyetumwa kuniongoza katika mafanikio.**

**SOMO LA ZIADA:** Yakobo 4: 6



**Warumi 13:11**
**"Naam, tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini......"**

Kuna neno la herufi kadhaa ambalo lina nguvu zaidi kuliko shida yoyote unayopata sasa hivi. Lina uwezo wa kuhamisha mtazamo wako kutoka kuwa wa kupungikiwa hadi kuwana utele, kutofaulu kuwa ushindi, ugonjwa hadi uponyaji, na kukata tamaa kuwa matumaini. Ni neno ambalo watu wengi hulihusisha na kuchelewa. Lakini limejawa matarajio, utele katika kutazamia, na mimba ya kiuwezekano. Ni nguvu ya "walakini." Ninapenda jinsi nabii Habakuki alivyosema. Alisema, " Ingawa mtini hauchanui maua na hakuna zabibu juu ya mizabibu, ingawaje mzeituni hauzai, na hata mashamba hayatoi chakula, iwapo hakuna kondoo katika banda, wala ng□ombe katika zizi, hata hivyo nitashangilia katika Bwana, nitamfurahia Mungu Mwokozi wangu " Haleluya! Ni nini kinachokupa ujasiri wa kutarajia hata wakati inaonekana hakuna kitu kinachosonga mbele katika maisha yako, wakati unazungukwa na kufeli, wakati hakuna kitu cha kuonyesha kama matunda ya bidii yako, wakati uchumi uko chini, wakati kuna wasengenyaji pande zote karibu na wewe? Ni Mungu wa wokovu wako! Yeye ni Baba mzuri, na matakwa yake kwako ni mazuri daima. Maadamu yuko maishani mwako na una uwezo wa kusikia neno Lake, unaweza na unapaswa kutarajia kila kitu kizuri. Chochote kinachoonekana kama haiwezekani ni uwongo. Amini tu, na utaona na kushuhudia wema wa Bwana.

## UKIRI WA KINABII

**Siwekewi ukomo na hali yangu ya sasa kwa sababu mimi ni mtoto wa Mungu asiye na ukomo. Kwa hivyo, ninatarajia mambo mazuri kutokea kwangu kila siku. Kamwe sitakosa fursa sahihi, na mimi kamwe sitanyimwa haki ya kuyafikia katika yaliyo yangu kwa haki ya kiungu. Mimi ni muwaza kiuwezekano na mfanya yasiyowezekana, na Mungu wangu atafanya zaidi ya kitu chochote Natarajia anifanyie.**

**SOMO LA ZIADA:** Habakuki 3:17; Warumi 10: 8,10



**1 Wakorintho 15:10**
**"Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami."**

Nataka kukupa siri ambayo itabadilisha namna unavyofanya biashara, huduma, mahusiano, na maisha kwa ujumla. Tunaamini kuwa na bidii katika biashara, na Bwana mwenyewe anatuamuru tufanye biashara mpaka atakapokuja. Lakini kuna haja ya kuwa na tofauti katika njia tunayofanya biashara kama Wakristo na jinsi ulimwengu unavyofanya mambo yake ya biashara. Kwa nini tuwe tunaomba mambo ambayo watu wa ulimwenguni wanayapata bila kuomba wakati kuna rasilimali ambazo zinatupa haki ya kufanya kazi kutokea kwenye nafasi ya mapumziko? Kuna faida ya kiungu inayopatikana kwako ambayo inakuweka juu maishani. Ni faida ya neema. Mtume Paulo anaiweka hivi: Nilifanya kazi nyingi kuliko wote, lakini haikuwa mimi, lakini neema ya Mungu. Haleluya! Unaweza kuiajili neema kukufanyia kazi. Neno la Mungu linasema kwamba unapoyafanya mambo ya Ufalme kuwa kipaumbele chako, " neema yote (kila upendeleo na baraka za kidunia)" inapatikana kwako. Kama mtoaji, unajiweka sawa ili kila aina ya neema - kila upendeleo na baraka za kidunia - ikufanyie kazi. Kuna neema ya kupokea mawazo ya kibiashara yanayoleta faida, neema ya kupata wateje wa kuwahudumia, neema ya kuipeleka biashara yako kwenye kiwango kingine, neema ya masoko na mauzo, neema ya bidhaa na huduma zako kupendwa na kununuliwa, na neema iliyopendekezwa ya upanuka, neema ya kutawala tasnia yako, neema ya kupata mwenzi mzuri, neema ya kushika mimba. Kuna kila aina ya neema! Kila neema inatwaliwa kwa imani. Unahitaji kuamini tu na kutamka neema unayotaka kuona inafanya kazi katika mambo yako. Chochote kinachohitajika, kuna neema kwa ajili yake.

## UKIRI WA KINABII

**Nakataa kupambana. Kwa neema ya Mungu, nafanya mambo kutoka kwenye nafasi ya kupumzika. Nimepakwa mafuta ya ubora na ushawishi katika soko. Mimi ni sumaku ya rasilimali. Kibali kinayavuta mahusiano sahihi kwangu. Nina neema ya kuzaa matunda; hakuna utasa katika maisha yangu. Bidhaa zangu zinahitajika sana, huduma zangu ni muhimu, mikataba ya biashara inaanza kunipata, napata wateja kwa urahisi, na pesa zinapiga hatua kuelekea kwenye akaunti yangu ya benki.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 9: 7- 8 AMPC; 2 Wakorintho 4:13; Waebrania 4:16



**Waebrania 11: 3; 2 Wakorintho 4:13**
**"Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena"**

Jumba la sanaa limejazwa na kazi za sanaa ambazo haziwezi kupatikana kila mahali. Ndiyo sababu watu watasafiri kutoka mbali ili kusimama tu na kuzitazama zikiwa wametundikwa ukutani. Ni jukumu la mwangalizi kutambua kwa umakini, kuchagua, na kukusanya zilizo bora zaidi, kisha azipange ili mpangilio wake ubebe dhamira uliyokusudiwa. Vivyo hivyo, Mungu amekupa nguvu ya kutengeneza maisha yako. Unalifanyaje hilo? Kwa kutambua kwa umakini, kuchagua, na kukusanya maneno bora, kisha kuyapangilia ili muonekano wa maisha yako uwe vile unavyotaka iwe. Maneno yako yanaunda maisha yako. Hii ndiyo sababu muhimu sana kwamba ufanye kwa umakini sana - kufahamu na kukusudia - kuhusu unachokisema. Usiongee sana. Badala yake, tambua kwa uangalifu na uchague maneno ambayo yatakuletea faida zaidi. Kuna mambo ambayo Mkristo anapaswa kusema, na vitu ambavyo Mkristo hapaswi kusema kamwe, kwa sababu kile unachosema, kinaumba. Hivi sasa, maisha yako ni zao la maneno ambayo uliyasema na maneno ambayo "uliyatazama" na kuyaamini. Ikiwa maisha yakohayako kabisa kama vile unavyoyatamani kuwa, habari njema ni kwamba unaweza kuyabadilisha. Kuwa mtunza neno. Hivi sasa, unaposoma maneno haya, unapokea neema - upako - kutambua ni maneno yapi yanafaa kwa jumba la sanaa ya maisha yako na ambayo hayafai.

## UKIRI WA KINABII

***Mimi ni mtunza neno. Maneno yangu yamekusudiwa na yana nguvu. Ninaposema, natamka kama Mungu anavyotamka na kuyaleta katika uhalisia mambo ninayoyataka. Kwa hivyo, kabla ya kusema, ninaifanya akili yangu iwe na nia ya Kristo, na kwa uangalifu natambua, nachagua, na nayaumba kwenye akili yangu maneno ambayo yananufaisha mimi na wale wanaonizunguka. Maisha yangu ni kazi ya sanaa, na mafanikio yangu yamehakikishiwa.***

**SOMO LA ZIADA:** Yohana 6:63; Wakolosai 4: 6



**Warumi 12:18**
**"Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote"**

Kuna watu ambao ni ngumu kushughulika nao, na watakuwa hivyo daima. Wao ni wa asili wenye wagonvi na wanaoneka-na kustawi panapokuwa na makwaru-zano. Haijalishi unafanya nini au haufanyi nini, wanapata njia ya kusababisha taa-bu na kuwadhuru wengine kwa maneno yao. Mstari wetu wa leo unadokeza ukweli kwamba haiwezekani kila wakati kuishi kwa amani na kila mtu. Lakini kuna ufun-guo ambao unatujulisha ni mahali gani tunapaswa kufanya kwa sehemu yetu kama Wakristo. Kwanza, lazima tuelewe kitu juu ya maana ya kuishi "kwa amani." Kuishi kwa amani kunamaanisha kufanya amani, kukuza au kudumisha amani, na kuwa au kuishi kwenye amani. Maana mbili za kwanza zinahitaji ushiriki wa anga-lau mtu mwingine mmoja. Ukweli ni kwamba, unaweza kutamani amani, laki-ni mtu huyo mwingine akawa hataki. Ndio maana Mtume Paulo anaingilia ki-fungu muhimu, "kadiri alivyo ndani yako." Huwezi kudhibiti kile watu wengine wanafanya au jinsi wanavyoitikia kila hali. Lakini unao udhibiti kamili juu ya jinsi unavyochagua kuitikia. Unaweza bila kikwazo chochote, kuwa na amani kila wakati. Ni asili yako na haki ya kufanya hivyo. Mateso, wanasema, anapenda mshirika. Lakini mateso kamwe hatastarehe kwenye ushirika na wale wana-ochagua amani.

## UKIRI WA KINABII

**Ninampenda kila mtu kwa sababu upendo ni asili yangu. Sisemi mabaya kwa mtu yeyote kwa sababu nimekataa kuacha nguvu yangu au amani yangu. Haijalishi ni maneno gani mabaya yanayo-semwa juu yangu, sitajibu jibu lisilo la upole. Nakataa kusumbuliwa na maneno au matendo ya wengine. Ninachagua kuishi kwa amani kwa sababu amani ni urithi wangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:27; Wagalatia 5:22; 1 Petro 3:11



**Matthew 10:31**
**"Msiogope basi; bora ninyi kuliko mashomoro wengi."**

Fort Knox inachukuliwa kuwa mahali panapolindwa kwa hali ya juu zaidi Duniani. Ikiwa kwa namna fulani unaweza kuwapita askari 30,000 wanaolinda nje, lazima ujue jinsi ya kuupita kuta. Kuta hizo zimetengenezwa kwa matale, unene wanfuti nne, na imeshikiliwa pamoja na tani 750 za chuma na saruji. Imejengwa kuhimili aina yoyote ya mashambulizi. Kwa kweli, inaaminika kwamba kuta zimeimarishwa vizuri kiasi cha kuweza kuhimili kugongwa moja kwa moja na bomu la atomiki. Ndani, ukifanikiwa kuupita ukuta kuna milango iliyofungwa, utakumbana na mlango wa kuba tani 22 ambapo watu wachache kila mmoja anashikilia kipande cha nywila. Hakuna mtu mmoja anayejua nyila nzima. Inalindwa na teknolojia ya usalama ya hali ya juu Zaidi. Hii yote na zaidi ni kulinda dhahabu iliyomo ndani. Dhahabu haiwezi kufikiria, kuongea, au kuona. Haina roho au nafsi. Haina hisia, na haiwezi kupenda. Walakini, inalindwa na kutunzwa kwa kiwango kile kilichokithiri. Je! Wewe si zaidi? Mungu aliye muumba wa dhahabu aliona kwamba hakuna kiasi cha dhahabu ambacho kitafaa kikilinganishwa na hadhi na thamani yako kwake. Kama mtu anaweza kwenda kiwango cha mbali kiasi kile kulinda vitu visivyo na uhai, tunajua kwamba Baba yako wa Mbinguni hakuacha wewe bila ulinzi au kinga. Wewe ndiye umiliki wake wa thamani sana, wala hutaondoshwa kamwe.

## UKIRI WA KINABII

**Kila hatari ninayokabiliwa nayo, ninashinda vita hiyo katika Jina la YESU! Hakuna mtu atakayeniondoa kwenye kiti cha enzi kutoka mahali ambapo Mungu ameniweka. Siwezi kamwe kushushwa daraja. Naendelea kupanda juu, na hakuna unayeweza kuniondoa kutoka kile Yeye ameniinua kwacho.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8: 31-39



**1 Timotheo 6:16**
**"ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina."**

Dini za ulimwengu zina kitu kimoja cha ufanano. Vyote vinakufundisha kwamba kuna kitu lazima ufanye ili kumpata Mungu. Ukristo hauko hivyo. Misingi ya imani yetu inafundisha kwamba haiwezekani wewe kumfikia Mungu kwa juhudi zako mwenyewe. Andiko letu la leo linatuambia wazi kwamba hakuna mtu anayeweza kumfikia. Anaishi katika nuru isiyoweza kufikiwa ambayo hakuna mtu anayeweza kuona au au amewahi kuona. Mungu, kwa maana hiyo, hawezi kufikiwa na mwanadamu. Hii inaweza jambo la kukatisha tamaa, lakini kwa Mkristo, ni habari ya kufurahisha zaidi.Unaona, Mungu alifanya kitu bora kuliko kutufikia sisi. Alitufikia mwenyewe. Akijua kuwa yuko katika umbo ambalo huwezi kuligusa, alikuja katika umbo ambalo unaweza kugusa katika Nafsi ya Yesu. Hatukuweza kumtazama katika umbo lake halisi, kwa hivyo alijimwaga ndani ya mwili wa mwanadamu na kutangaza "Mimi ndiye Nuru" ambaye tunaweza kumtazama. Yesu ni mnyambuliko wa upendo wa Mungu kwako. Yeye hauzuii wewe kuikaribia nuru hiyo. Njia pekee unayoweza kuikaribia ni kutoka ndani yake. Biblia inasema kwamba maisha yako yamefichwa na Kristo ndani ya Mungu. Ukiwa ndani ya Kristo, haukaribii tena nuru hiyo isiyoweza kufikiwa. Uko ndani yake.

## UKIRI WA KINABII

**Ninafanya kazi kutokea mahali pa mwangaza. Uelewa wangu umeangaziwa, na kunifanya niwe na ufahamu kamili, kutunza kumbukumbu, na kuelewaa. Nimeingiziwa nuru, na maisha na nguvu za Mungu zimejaa kila seli, zinaondoa kuumwa na magonjwa kutoka kwenye mwili wangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA:** Matendo 17:28; Wakolosai 3: 3



**Warumi 12: 2**
**"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu…"**

Wengine wanafikiri ustawi wa kifedha sio kwa ajili ya Wakristo. Hawako sahihi kabisa. Mungu alijitambulisha na watu watatu katika Biblia - Ibrahimu, Isaka, na Yakobo - na kila mmoja wao alikuwa tajiri mkubwa. Katika Kutoka 3: 6, Mungu alimwambia Musa, "… Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo " Mwanzo 13: 2 inatuambia kwamba Abrahamu "alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu." Biblia inasema hivi kumhusu Isaka mwanawe, " Na mtu huyu [Isaka}akawa mkuu, akazidi kusitawi, hata akawa mkuu sana. Akawa na mali ya kondoo, na mali ya ng'ombe, na watumwa wengi. Hao Wafilisti wakamhusudu. "(Mwanzo 26: 13-14). Yakobo, pia, alikuwa na ushuhuda kama huo. Biblia inasema," Kwa hiyo mtu huyo [Yakobo] akazidi mno, akawa na wanyama wengi, na vijakazi, na." (Mwanzo 30:43). Ustawi wa Mungu sio kwa wateule wachache; ni kwa wale wote wanaofuata na kuishi kwa Neno lake. Alisema katika 3 Yohana 1: 2, " Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo." Ikiwa umekuwa ukipambana kila wakati na maisha ya ukosefu, uhitaji, na umasikini, unachohitaji ni mwelekeo mpya, mtazamo mpya. Badilisha lugha yako, ufahamu, na mawazo, na hali yako itabadilika. Warumi 12: 2 inasema, " Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu " Fikiria na uzungumze ustawi hadi mawazo yako yote sio tu yaburutwe lakini pia yameingiziwa na uwezekano wa maisha ya mafanikio.

## UKIRI WA KINABII

**Ni mapenzi ya Mungu kwangu kuwa tajiri, sio kwa ufunuo tu bali pia kwa pesa na hazina za kifedha. Mimi ni mrithi wa Mungu na mrithi pamoja na Kristo. Nilizaliwa katika familia tajiri zaidi Duniani, na mafanikio ni haki yangu ya kuzaliwa. Kwa hivyo, nina na kudumisha fahamu ya utoshelevu na utele uliokithiri. Utajiri wote katika ulimwengu huu ni wangu!**

**SOMO LA ZIADA:** Zaburi 112: 1-3; Warumi 8:17; 1 Wakorintho 3:21



**2 Petro 1: 3-4**

**' Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. '**

Mungu anaweza kugeuza maji kuwa divai, lakini hawezi kugeuza kunung'unika kwako kuwa ushindi. Kama mtoto wa Mungu unapopitia changamoto, usilalamike! Bwana alijua kutakuwa na changamoto, lakini alitupa hakikisho kwamba tutashinda daima: Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. Mbele ya shida jifunze kutokulia, jifunze kutokulalamika bali uwe kama Mtume Paulo kama katika andiko letu la ufunguzi ambaye alimshukuru Mungu, aliyekuwa mdhamini wa ushindi wake. Mtume Paulo hata alimshukuru Mungu kwa ushindi unaokuja. Aliupalilia mtazamo wa kiushindi, alijua kwamba angeweza kufanikisha na kufanya chochote kupitia Kristo ambaye anamtia nguvu. Usifikirie kushindwa, kufeli au udhaifu, mshukuru Mungu kwa ushindi wa zamani na wa sasa na uwe na shukrani kwa matendo ambayo Mungu tayari anafanya katika maisha yako. Mtu ambaye amejawa na shukrani ni mtu wa ushindi mara zote.Tambua ukweli kwamba kusudi la Mungu kwa maisha yako ni kukupa ushindi. Neno kukupa ni neno la Kiyunani DIDOMI [kusambaza, kuwezesha, kumpa mtu kitu kwa faida yake] Ushindi wako ni ukweli ambao umeshapangwa tayari. Hakuna kitu ambacho ni, na kinaweza kuwa kwa hasara yako. Ushindi utokao kwa BWANA hautaacha dalili yoyote ya uwepo wa adui maishani mwako. NI USHINDI WA KUDUMU. Mtoto wa Mungu tembea katika ukweli huo na hautasumbuliwa na changamoto za maisha.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni raia wa Sayuni, nimezaliwa mara ya pili na maisha ya namna ya Mungu. Sheria ya dhambi na mauti imetanguka na ni batili maishani mwangu. Kwa hivyo, mimi siwezi kuumwa na kuwa na magonjwa, kushindwa, au kuwa maskini. Sheria ya Roho ya Uzima inafanya kazi katika mwili wangu na katika akili yangu, kwa Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA:** Mathayo 8: 16-17; Warumi 8: 2, 11




**BECOME A UAF PARTNER TODAY BY VISITING**
**WWW.UEBERTANGELFOUNDATION.ORG**

UEBERTANGEL
FOUNDATION





**Luka 17: 14-1 6**

**'Alipowaona aliwaambia, Enendeni, mkajionyeshe kwa makuhani. Ikawa walipokuwa wakienda walitakasika. Na mmoja wao alipoona kwamba amepona, alirudi, huku akimtukuza Mungu kwa sauti kuu; akaanguka kifudifudi miguuni pake, akamshukuru; naye alikuwa Msamaria. '**

Tumeona miujiza isiyo na hesabu ikifanyika kwenye wa huduma zetu. Watu wamepokea notisi za miujiza ya fedha zilizoingia katika akaunti zao za benki, kadi zao kwa ajili ya manunuzi kuongezewa pesa, miamala ya pesa kwenye simu zao, fedha kuonekana katika mifuko ya nguo ya watu. Miujiza inayotokea haiwezi kukanushwa na mara nyingi watu huitikia kwa machozi ya furaha au kelele za sifa kwa Bwana. Lakini watu hao wasingejua miujiza iliyotokea ikiwa hawangeangalia mifuko yao, mkoba, pochi au kuangalia kadi zao za benki. Vivyo hivyo wakati uponyaji unafanyika. Mpokeaji ataagizwa kufanya kitu ambacho hawangeweza kufanya hapo awali. Kulikuwa na mwanamke mmoja ambaye alipokea muujiza mkubwa wa uponyaji. Tumbo lake lilikuwa limevimba kama mjamzito. Uponyaji ulipoachiliwa kwake, hakugundua hata kwamba muujiza ulikuwa umefanyika. Ilibidi mtu mmoja aeleze kwamba tumbo lake limekuwa sawia kabisa. Kile ni kweli kuhusu pesa za miujiza, kadi za fedha za miujiza, na uponyaji, ni kweli kwa kitu chochote ambacho umelenga imani yako kupokea. Lazima ufuatilie muujiza wako. Wale wakoma kumi katika andiko letu la leo wote walipokea uponyaji, lakini tunaambiwa ni mmoja tu wao "aliyeona kwamba ameponywa." Haikusema alihisi au kusikia chochote cha kuvutia. Alikuwa akilenga tu kile kinachoweza kutokea katika mwili wake - akitafuta mabadiliko - na akaona. Usikose udhihirisho wa muujiza wako kwa sababu unasubiri kitu Fulani cha kushangaza kutokea. Mara tu baada ya kupokea Neno kuhusu suala lako, anza kutafuta dalili yoyote ya kitu kufanyika. Hata kama ishara za mwanzo zinaonekana kwenda kinyume na matokeo unayotarajia, anza kumpa Mungu utukufu, kumshukuru kwa muujiza ambao umefanyika, na hakika utarudi na ushuhuda.

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yanabadilika katika maisha yangu hivi sasa. Ninafanya Neno la Mungu litimie, na ninaamuru na kutangaza uhai kwa kila hali iliyokufa.**

**SOMO LA ZIADA:** Luka 17: 11-19



**Waebrania 11: 1**
**"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."**

Imani ni ya muda mfupi. Wakristo wengi hawajafundishwa hivyo. Matokeo yake, Wakristo hao wamekuwa wakijaribu kupata matokeo kwa imani ambayo haifanyi kazi tena. Biblia inatuambia kwamba imani ni bayana ya mambo yatarajiwayo. Ni muundo ambao hufanya jengo kuu kusimama kwa vitu ambavyo unataka kuwa navyo ambavyo bado haujaona na macho yako ya mwili. Ukisha kuiona, hauitaji tena imani kwa ajili yake. Imani ni ya muda kwa msingi huo. Jambo kuu unalohitaji kujua kuhusu imani ni kwamba huwezi kutumia imani ya jana leo, na huwezi kuitumia imani ya leo kesho. Imani lazima iwe sasa. Andiko letu la leo linasema "imani ni," sio imani "ilikuwa" au imani "itakuwa." Na kulingana na Warumi sura ya 10, aya ya 17, imani hiyo "huja" kwa kusikia. Imani inapaswa iendelee kuja, na inaweza kuendelea kuja tu pale unapoendelea kusikia. Imani haiji kwa kusikia Neno la Mungu. Inakuja na ustadi wa kusikia, mchakato wa kusikia. Mchakato huo wa kusikia huja kwa Neno la Mungu. Kwa maneno mengine, Neno la Mungu huja na kuzalisha kusikia ndani yako, na aina hiyo ya kusikia inaleta imani. Chukua muda kusikia Neno. Ni kwa ajili yako ili kukusaidia sasa.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtenda Neno. Sisikii tu Neno, bali naenda zaidi ya kusikia kwa kutenda yale niliyosikia. Imani ni mtindo wangu wa maisha. Nimepewa nguvukasi kusababisha mabadiliko na kushinda hali yoyote ya maisha.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 10:17; 1 Yohana 5: 4



**Warumi 12:19**
**"Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, Kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa, anena Bwana."**

Kama Wakristo, hatufurahii anguko la wale wanaotupinga au wale wanaojisimamisha wenyewe dhidi yetu. Hiyo haingeonyesha tabia ya Kristo ndani yetu. Badala yake, furahi kuwa unajulikana na Mungu na unaishi ndani Yake, na asili yake inafanya kazi ndani yako. Katika huduma, tumekutana na watu wa kutusumbua bila hata sababu, wakisema kila aina ya mambo juu yetu. Kile wasichotambua ni kwamba tunachochewa, tunaamshwa, na kutawaliwa na upendo. Upendo unapokutawala, inakufanya uwe bwana katika maisha. Hakuna kinachokuhamisha. Hakuna kinachosababisha usumbuke. Wakati wana wa Israeli walipotoka Misri, walipora utajiri wa Wamisri. Waliishi Misri wakiwa maskini, lakini walitoka wakiwa na mafanikio na udhia. Kama mtoto wa Mungu, umekusudiwa kufanikiwa, na kwa mafanikio kunakuja udhia. Lakini udhia unapokuja, usilipize kisasi. Usiseme mabaya kwa mtu yeyote. Maadui zako wanapokufukuza, dumisha fokasi yako na endelea kusonga mbele. Kama Mungu alivyowaondolea magurudumu kwenye magari ya wale ambao walikuwa wakiwafuatia wana wa Israeli, Mungu wako ni uwezo wa kupunguza kasi ya adui. Yeye ni Yehova Gmolah, Mungu anayelipa. Mtu yeyote anayepambana na wewe anapigana na Mungu anayekufanikisha, na hiyo ni vita ambayo hawawezi kushinda kamwe.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha marefu ni yangu, kwa Jina la Yesu. Sitakufa. Roho wa Mungu humfukuza kila mharibifu anayelenga kuniangamiza. Kila jitu linalonizuia linatawanyika sasa hivi. Adui yeyote - iwe ni kifedha, ugonjwa, au kitu chochote kinachotaka kusimama katika njia ya maendeleo yangu - ameondolewa sasa kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Kutoka 14: 21-25; Mithali 24:17



**Yuda 1:20**
**"Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu"**

Siku ziliyopita, tulizungumza juu ya jinsi imani ilivyo sasa, na jinsi imani "inavyokuja" kwa kusikia inahitaji sisi kuendelea kusikia Neno la Mungu juu ya jambo tunalotamani kubadilisha. Tunasimama chini ya Neno hilo mpaka tutakapoona madhihirisho. Ingawa huwezi kutumia imani ya jana leo, kuna namna ya kuinua imani yako kwa kiwango fulani na kamwe usishuke tena. Kwa njia hiyo, wakati lengo lako la imani ijayo limewekwa, sio lazima uanze tena chini kujenga imani yako. Unaweza kuanza katika kiwango cha mwisho cha imani uliyofikia. Imani ni kama ngazi ambayo haina mwisho kwenda juu. Hakuna kikomo cha kiwango gani unaweza kwenda juu, na ni Roho Mtakatifu anayekusaidia kutoka ngazi moja ya imani hadi nyingine. Unapoomba katika Roho Mtakatifu, Anakuongezea - kukujongezea kiwango kingine - kwa kunena kwa lugha, maneno ambayo hayawezi kutamkika katika usemi wa maongezi. Unaponena kwa lugha, unaweka imani yako mahali kwenye kiwango cha Neno au ufunuo uliopokea tu. Ni kama kulibana dirisha ili liwe wazi; imani yako haiwezi kushushwa. Tafuta muda wa kuomba. Na unapoomba kwa lugha, fahamu kuwa unaikaza imani yako - jiambie uko katika kiwango cha juu cha imani. Unaposoma vitabu vyetu, baada ya kusoma sura moja, omba kwa lugha. Unaposikiliza jumbe tunazofundisha na kuhubiri na kupokea ufunuo, omba kwa lugha. Unapofanya hivyo, unaweka imani yako katika kiwango kingine na kufungia ufunuo huo ndani ya roho yako.

## UKIRI WA KINABII

**Imani yangu inahamia ngazi nyingine. Ninapoomba katika Roho Mtakatifu, ninaomba kwa ujasiri nikijua kwamba ninaomba kutoka kwa kiwango bora na cha juu cha imani. Ninainuka kama jumba, juu hadi juu zaidi. Siwezi kuzuiliwa, mbadilisha ulimwengu, na ushujaa wangu pia utarekodiwa katika Jumba la Umaarufu la Imani.**

**SOMO LA ZIADA:**
Warumi 1:17



**2 Wakorintho 13:14**
**"… na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote."**

Roho Mtakatifu ni nafsi ya Mungu ambayo haieleweki vyema Zaidi kwa wengi, lakini Ndiye mmoja aliye pamoja na sisi Zaidi hapa duniani. Mara nyingi hushushwa kwa hadhi ya "kuwa kitu," au amepewa taaswira ya vitu kama nguvu au moto. Hufikiriwa wakati tu watu wanataka jambo la linalozidi kawaida au la ajabu lifanyike, kama kitu cha kutumiwa hivi. Lakini, Neno la Mungu linaonyesha wazi kwamba Roho Mtakatifu ni Mtu. Anaongea, Ana hisia, na nini zaidi, Yeye pia anataka sana mahusiano kama wewe unavyotamani mahusiano. Anatamani kuwa na mahusiano na Wakristo wote. La muhimu zaidi, anataka kuwa na mahusiano na wewe. Anataka kuongea nawe na kujadili mambo na wewe. Anataka kujumuishwa katika mazungumzo yako na kushiriki katika shughuli zako za kila siku. Na inaumiza hisia Zake anapopuuzwa.Ingawa Roho Mtakatifu ni Mungu, hauombi kwake. Badala yake, unaomba pamoja naye. Yeye ndiye mshirika wako mkubwa na anayeaminika wa maombi. Unapoomba, mwambie Roho Mtakatifu, "Wacha tuombe pamoja." Hii ndio maana ya kuomba katika Roho au kuomba kwa Roho Mtakatifu. Kuomba na Roho Mtakatifu haimaanishi unahisi Roho Mtakatifu karibu nawe. Kuomba na Roho Mtakatifu inamaanisha unamwambia kihalisi kabisa, "Wewe ni Mwenzangu, Mwandani wangu, rafiki yangu nd. Njoo tuombe pamoja." Unapokula, usimwombe Roho Mtakatifu akibariki chakula hicho. Badala yake, mwalike Roho Mtakatifu kula nawe, kisha omba na ubariki chakula chako. Habariki chakula. Badla yake Anakula chakula na wewe. Unaponunua, muulize mashauli yake juu ya nini unapaswa kununua. Kila asubuhi, tabasamu na useme, "Habari ya asubuhi, Roho Mtakatifu! "Msalimie alasiri. Zungumza naye katika siku yako yote. Na unapolala usiku, mwambie," Usiku mwema, Roho Mtakatifu. "

## UKIRI WA KINABII

**Roho Mtakatifu, wewe ni rafiki yangu kipenzi, na sifanyi kitu chochote bila Wewe. Nimeweka nia ya kuupalilia uhusiano wangu na Wewe. Kwa sababu yako, siko peke yangu kamwe. Wewe uko pamoja nami kila wakati na u karibu nami. Ninaendelea na maisha kwa ujasiri kwa sababu Wewe unanifundisha kila kitu ninachopaswa kujua ili kufikia kiwango cha juu kabisa cha mafanikio. Asante, Roho Mtakatifu, kwa kunipenda na kunisaidia katika yote ninayofanya. Ninakupenda!**

**SOMO LA ZIADA:** Yohana 16: 7; Yohana 14:26



**Waebrania 10:23**
**"Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu;"**

Kuna tofauti kati ya kukiri na kuthiitisha. Kukiri ni wakati unatangaza kitu ambacho unataka kuwa mkweli. Uthibitisho ni wakati unatangaza jambo ambalo unajua kuwa ni kweli. Hauthibitishi ili kupata. Unathibitisha kwa sababu tayari umepata. Biblia inazungumza juu ya kukiri kwa imani yetu, lakini neno hilo kwa kweli linamaanisha uthibitisho. Ni kukubali kile unachokimiliki tayari. Unapothibitisha kitu, ni zaidi ya maneno tu kutoka kinywani mwako. Unapothibitisha kitu, unahusisha mwili wako, unashirikisha hisia zako, na unazungumza kutoka kwenye roho yako. Uwewe wako wote unahusika, roho, nafsi, na mwili. Wewe ni tajiri. Huo ni uhalisia. Unapothibitisha kuwa wewe ni tajiri, hautangazi tu kama unavyoanza muda kwenye saa. Hapana! Unalazimisha mwili wako na nafsi yako iiambatane na ukweli wa Neno. Unatabasamu kwa sababu ya jinsi utajiri wako ulivyo. Unahisi ule uzuri wa kuwa tajiri unapofanya uthibitisho wako.Muhammad Ali alijisifia kuwa bondia mkubwa kuliko wote. Wakati bila shaka alikuwa bondia mkubwa, takwimu zake zilithibitisha hakuwa bora kufikia viango vya juu Zaidi vya ubora. Rekodi yake ya mwisho ilikuwa ushindi wa 56 kati ya mapigano 61, takwimu ambazo zilibadilishwa na mabondia wengine. Lakini kwa jinsi alivyokuwa anajiona, alikuwa mkuu kuliko wote, na hakuna mtu aliyeweza kumshawishi vinginevyo. Yeye mfululizo alithibitisha hilo. Kushinda au kupoteza - na kuna nyakati alipoteza - hakuna kitu kinachoweza kumfanya abadilishe au aache uthibitisho wake. Ndivyo unavyopaswa kuwa na Neno ambalo linakuambia ukweli juu ya wewe ni nani na unayo nini. Nenda sambaba na Neno kila wakati. Kamwe usiruhusu chochote kikuzuie kuthibitisha wewe ni nani na ni nini chako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaona malaika watakatifu wakinizunguka kila siku. Ninahisi malaika wamenizunguka. Siwezi kamwe kutembea peke yangu. Daima niko na Yesu. Mimi ni mamilionea. Mimi ni tajiri. Mimi nimefanikiwa. Siwezi kamwe kwenda chini. Siwezi kamwe kufilisika. Siwezi kamwe kuwa maskini. Mimi ni mkubwa kuliko kitu chochote ambacho kimewahi kutokea. Mimi kitu bora Zaidi kutokea duniani!**

**SOMO LA ZIADA:** Warumi 10:17



HabariNjema
KILA SIKU



**Matendo 1: 8**
**"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi"**

Wakristo wengi wanamuomba Mungu nguvu. Ukweli ni kwamba, bila kujali ni kiasi gani wanafunga, kuomba, kutangaza, au kumlilia Mungu, hatawapa nguvu hizo wanazoomba kwa sababu tayari walishapewa. Shida ni kwamba, hawajui nguvu ambayo tayari wanayo. Umeshapewa nguvu, dunamis, ambayo ilitafsiriwa kutoka kwenye Kiyunani inamaanisha nguvu ya asili - nguvu ambayo inakaa ndani ya jambo kwa sababu ya asili yake. Hii sio nguvu ambayo unahitaji kujaribu kupokea. Kama Mkristo, tayari unayo. Nguvu hii inakaa ndani yako, lakini haitakufanyia wewe au wengine wowote mema mpaka uitambue kwamba unayo. Nguvu ya Dunamis - nguvu uliyonayo - ni nguvu ya kufanya miujiza. Ni nguvu ya maadili na ubora wa nafsi. Ni nguvu na ushawishi ambao ni mali ya utajiri na ukwasi. Ni nguvu na rasilimali zinazotokana na nambari. Na ni nguvu ambayo iko na inayojumuisha majeshi, vikosi, au makundi. Nguvu uliyonayo ndani yako ni nguvu ya miujiza, uwezo, utele, nguvu, na uweza. Hausubirii nguvu. Wewe ni nguvu inayotembea, inayoongea tayari kukabili changamoto yoyote na kutimiza misheni yoyote.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mjumbe wa nyakati za mwisho wa ufalme wa Mungu niliyetumwa kuleta mabadiliko katika ulimwengu huu. Niko hapa kwa utume, na utume huo utatimizwa bila kufeli. Nimepewa nguvu ambayo inanifanya niwe mtu wa ushawishi, ubora, na uwezo.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Wakorintho 4:20; 2 Petro 1: 3



**Warumi 10: 6,8**

**'Bali ile haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi, Usiseme moyoni mwako, Ni nani atakayepanda kwenda mbinguni? (Yaani, ni kumleta Kristo chini), Lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo. '**

Kila kitu unachotamani tayari kiko hapa. Gari unayotaka, nyumba hiyo ya vyumba vinne unayoiangalia unapopita kila jioni, pesa zote unazoweza kubeba, kwa kuvitaja vichache. Mungu hakitumi chochote kati ya hivyo kutoka kwenye makao yake au kumtuma malaika Gabrieli kukuletea mlangoni pako. Tayari amekupa kila kitu unachohitaji. Lakini unasema, ninahitaji pesa. Ninahitaji uponyaji. Nahitaji ndoa yangu irejeshwe. Ninahitaji visa yangu ya kudumu. Je! Ni wapi Mungu amenipa kila kitu ninachohitaji? Jibu ni rahisi: Neno ndilo unalolihitaji. Watu wanataka niwatabirie nyumba au visa, lakini una kitu bora kuliko mimi kukutabiria. Una Neno la Mungu, ambalo yeye Biblia inasema ni neno la uhakika zaidi la unabii. Kwa kweli, manabii ambao ni wa Mubgu husema Neno la Mungu. Sharti kuu la neno lililosemwa kwako na nabii wa kweli ni kwamba ukae katika Neno. Neno kinywani mwako ni bora kuliko Yesu kushuka kutoka Mbinguni. Huo ndio usemi wa imani yako, na kwa wale wanaoshughulika na imani, Neno tu linatosha. Amini Neno la Mungu tu na uliseme kwa imani. Basi, hauwezi kamwe kuhitaji unabii.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha yaliyotabiriwa. Nikiwa nimejivika silaha ya Neno la Kweli, ninaamuru mambo na kuyafanya kuwapo. Siko katika hali ya kuchakazwa ya hali za maisha; Ninazitawala. Ninapotamka kwa imani, bunge la Mbingu linaniunga mkono, na neema inayofanya kazi maishani mwangu haitafanya neno langu lolote lianguke chini.**

**SOMO LA ZIADA:** Mathayo 14: 17-



**2 Wakorintho 9: 7**
**"Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu."**

Kuna tofauti kati ya kuwa muhimu na kuwa wa thamani. Sote ni wa thamani kwa Mungu, lakini si wote ni wa muhimu. Biblia inatuambia kwamba Mungu alimtuma Mwanawe afe kwa ajili ya ulimwengu wote. Ndivyo kila mtu alivyo wa thamani kwa Mungu. Lakini kuna wengine wanamudu kuongeza thamani yao kutoka kwa mtazamo wa Mungu na kuhitimu kutoka kuwa wa thamani hadi kuwa muhimu kwake. Andiko la leo linakupa njia rahisi ya kupata kadi ya VIP - Mtu Muhimu sana - orodha ya kipekee ya Mungu. Kuna kitu ambacho Mungu huthamini kuliko vitu vingine vyote: zaidi ya kuhubiri, zaidi ya kutabiri, zaidi ya maombi, hata zaidi ya kuvuna roho za watu, na huyo ni mtoaji mkunjufu. Unaona, pesa ni chombo cha kusukuma ajenda za Ufalme wa Mungu ziende mbele. Mungu mwenyewe alitangaza kwamba pesa husababisha miji yake kuenezwa nje, sio maombi, sio kuhubiri, sio kutabiri - pesa! Yesu alizungumza zaidi kuhusu pesa kuliko hata kuhusu Mbinguni na Kuzimu pamoja. Kwa hivyo, unakuwaje VIP kwa Mungu? Kuwa mtoaji ambaye haitoi tu kwa sababu mhubiri amekuomba utoe, lakini yule anayetoa kama Roho Mtakatifu anavyomwongoza wakati wowote. Na unapotoa, furahia na uwe mwepesi kutoa. Anafurahia katika yule anayetambua umuhimu wa kushirikiana naye ili kutimiza makusudi yake duniani anafurahia kufanya hivyo. Mungu anapenda sana, anafurahishwa naye, na hayuko tayari kumtelekeza au kufanya jambo bila mtu kama huyo. Mtazamo wako katika kutoa inaweza kuwa sera yako bora ya bima. Inaweza kukuhakikishia nafasi ya kudumu kwenye orodha ya VIP ya Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimekusudia katika akili na moyo wangu kuwa mtoaji. Nimepakwa mafuta kutoa, na ninapofanya hivyo, ninaunganisha kusudi langu na Mbingu na kutimiza agizo langu la ukuhani. Ninaleta furaha kwenye moyo wa Baba na kusababisha Injili kufika mwisho wa Dunia. Mimi ni VIP wa Mungu, na ninaenda popote bila woga kwa sababu Mungu hayuko tayari kufanya bila mimi, mtoaji wake wa haraka, mtoaji mchangamfu.**

**SOMO LA ZIADA:** Zekaria 1:17



**1 Wakorintho 3:21**
**"Basi, mtu ye yote na asijisifie wanadamu. Kwa maana vyote ni vyenu"**

Nchi chache sana zina mifumo yao ya alama ya mkopo. Ni mfumo ambao habari za kifedha za mtu binafsi hufichuliwa kwa taasisi fulani za kukopesha ili kuamua ni nzuri au mbaya ya hali yako ya kifedha. Alama za mkopo zinaweza kuathiri kiwango na masharti ya mikopo, gharama ya bima, na pesa ngapi zinahitajika kwa amana kwenye nyumba, huduma, au vitu vingine. Ikiwa alama yako ya mkopo ni ya chini, unabakiwa na uwezekano mdogo sana, ikiwa itazingatiwa. Ikiwa alama yako ya mkopo ni kubwa, fursa nyingi zaidi za kifedha zinapatikana kwako na kwa viwango bora. Ndio maana alama za mkopo za miujiza zimekuwa moja ya miujiza inayotafutwa sana katika huduma yetu. Lakini kuna kitu bora zaidi kuliko alama za mkopo za miujiza. Kinaitwa neema. Mungu hakuangalia alama zako za mkopo ili kubaini atakachokupa. Haangalii utendaji wako wa zamani au wa sasa kuamua ikiwa wewe ni bora kiasi cha kutosha kufuzu vitu unavyotaka. Amekustahilisha kwa wema Wake mwenyewe na kukuweka mahali pa kuwa sawa na Yeye kwa kukupa haki Yake mwenyewe. Mkusanyiko pekee kwenye rekodi yako ni wema na rehema. Kwa njia ya neema yake, alifanya iwezekane kwa wewe kupata chochote unachokitamani. Usiangukie katika mtego wa kufikiria kwamba majibu ya Mungu yanahusishwa na utendaji wako. Jamii inaweza kuwa imekuweka chini na kusema kuwa haukufai vya kutosha, lakini Mungu amekuinua. Umestahilishwa kwa neema yake, na kila kitu ni chako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamuru jambo na kulifanya kuwa hivyo kwa Neema ambayo inafanya kazi maishani mwangu. Nipo juu na kusonga katika kimo cha juu sana. Hakuna mtu anaweza kunishusha thamani kwa sababu Mungu amenistahilisha. Kwa hiyo, hakuna milango iliofungwa katika maisha yangu, kwa kuwa Neema ya Mungu amenipa kuyafikia yote, na sitakataliwa.**

**SOMO LA ZIADA:** Warumi 8:32



**1 Wakorintho 11: 1**
**"Igeni mfano wangu, kama ninavyouiga mfano wa Kristo" NEN**

Kuna mitindo mingi lakini sio waanzisha mitindo wengi, kwa sababu ni jambo gumu kuweka kiwango ambacho watu wengine wanataka kukifuata. Inahitaji neema fulani kufanya hivyo. Kwa mfano, unajua kwamba mtindo ya mavazi sio kipaji chako, jambo bora ni kumpata mlezi - mtu ambaye amejua sanaa ya mitindo - na unaiga mtindo wao. Angalia jinsi wanavyoweka mambo pamoja, wanadimamaje, jinsi wanavyojongea, wanaongeaje, na hata jinsi wanavyoongea. Huna haja ya kuunda upya gurudumu na kujaribu kujua jinsi ya kuanza mwelekeo mpya. Vivyo hivyo katika uwanja wa kifedha. Unapotaka kufanikiwa katika eneo fulani la biashara, tafuta mtu ambaye ameziteka pesa na kufikia kiwango fulani cha utawala wa kifedha. Jifunze ubora kutoka kwa waliobora, kwa sababu ubora unaigwa. Ndivyo ilivyo pia katika huduma. Ndio maana Mtume Paulo aliweza kusema kwa ujasiri, mnifuate mimi, kama ninavyomfuata Kristo. Alijua kwamba alikuwa amebeba neema fulani ambayo hakuna mwingine alikuwa nayo. Alikuwa amefundishwa binafsi na Bwana Yesu Kristo moja kwa moja, na alikuwa na njia fulani ya kuwasilisha Injili, mtindo na namna fulani ya kuongea. Sababu kuu ya makanisa kutokua ni kwamba kuna viongozi wa huduma ambao huweka haiba zao kwenye huduma wakati ilikuwa haiba ya mlezi wao ambayo hapo awali iliwavutia watu. Hatuna muda mwingi kabla ya unyakuo kutokea. Sasa zaidi ya hapo awali, lazima utumie faida ya neema ambayo imepatikana. Nakili mlezi wako. Mwamini yeye ambaye Mungu amemtuma. Fanya kile mlezi wako anafanya, na utapata matokeo kama ya mlezi wako.

## UKIRI WA KINABII

**Wingu ambalo liko juu ya maisha ya mtumishi wa Mungu aliye kwenye maisha yangu, lililo juu ya maisha ya familia zao, lililo juu ya mamilionea katika huduma yetu, wingu linaliwasababisha wazidi kupaa Zaidi liko juu yangu. Neema ya uponyaji iliyo katika huduma hii iko juu ya maisha yangu. Neema ya kueneza iliyo juu ya huduma hii iko juu ya maisha yangu. Kila wingu la kufanya kazi liko nami sasa katika Jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Waefeso 5: 1; Matendo 4:13



**2 Wakorinthо 4:18**
**"tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele."**

Kuna fumbo ambalo lipo katika maisha ya Wakristo wengi. Kwa mtazamo halisi, wanaonekana kuwa wamefilisika. Wanaangalia akaunti zao za benki, na hakuna mkato hata mmoja katika salio la akaunti za benki zao wa kuongelea. Kuna tu kama vileidadi ya namba za Utatu. Hiyo ni ukweli. Uhalisia, hata hivyo ni kwamba, haiwezekani wewe kama Mkristo kuwa fukara. Lakini mpaka uwe umeamka juu ya ukweli huu, ni kama mtu anayeingia dukani na mamilioni kadhaa katika akaunti ya benki lakini hajui kama ni yake. Anazunguka akifikiria hana rasilimali kupata kile anachotamani, wakati ukweli, angeweza kumiliki duka lote na mtaa wote lilipo duka hilo.Ni muhimu kwako kuelewa kuwa kuna tofauti kati ya ukweli na uhalisia. Ukweli umejikita katika hali za muda kidunia, vitu tunavyoona ambavyo vinaweza kubadilishwa. Lakini Kweli kwa ufafanuzi maana yake ni daima na habadiliki. Biblia inasema kwamba imani huja kwa kusikia. Kusikia, kwa upande wake, hutoka kwenye Neno la Mungu ambalo ni kweli – thabiti na lisilobadilika. Imani inapatikana kila wakati katika maisha ya Mkristo. Hiyo inamaanisha kuwa kila wakati una kile unachohitaji kubadilisha hali zako. Imani ni sarafu ya ulimwengu wa kiroho, na wewe ni kamwe hujawahi kutokuwa nayo. Ni zawadi uliyopewa na Mungu, na hataiondoa kamwe. Kamwe huwezi kufilisisha imani.

## UKIRI WA KINABII

**Nina kila kitu ninachohitaji kupata muujiza wangu. Kwa imani yangu, napata uponyaji. Ninasema kwa imani na kufufua chochote kinachoonekana kimekufa maishani mwangu. Kwa imani, naziita fedha katika uhalisia, nafaulu mitihani yangu, napata nyumba mpya, napata jengo jipya, napanda kanisa langu au shina langu, napata mke, napata ndoa yangu, na kupokea mtoto. Mimi sio mtu aliyekosa matumaini wala mnyonge. Mimi ni tajiri sana katika imani, na haiwezekani kwangu kufilisika.**

**SOMO LA ZIADA:** Waebrania 11



**Waefeso 2: 8-9**
**'Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. '**

Katika Olimpiki, moja ya mashindano kuogofya zaidi ni triathloni. Yanajunisha kuogelea, mbio ndefu, na wanaobanwa katikati ni wale wa baiskeli. Katika mguu wa baiskeli wa mbio, washindani hutumia mkakati wa kupendeza unaoitwa kujivuta, kanuni ya fizikia ambayo hupunguza upinzani. Kanuni ya kimsingi ya kujivuta ni kwa kadri unavyomkaribia mwendesha baiskeli aliye mbele yako, ndivyo unaokutana na upinzani mdogo wa hewa. Upinzani wote utakaokumbana nao unakabiliwa na mwendeshaji baiskeli anayeongoza aliye mbele yako. Matokeo yake, ni kwamba unafanya kazi kidogo, unatumia nguvu kidogo, na kufaidika kwa sababu ya kazi ya mwendesha baiskeli aliye mbele yako. Neema, kama mwendesha baiskeli anayeongoza au nahodha katika mbio za baiskeli, anayekuja kukupa faida. Inatengeneza njia ya upinzani mdogo kwa ajili yako. Kama unajikuta unachoka na kutumia nishati isiyo ya lazima, hiyo ni ishara kwamba unafanya kazi yote wakati neema inapaswa kufanya kazi kwa ajili yako. Badala ya kujaribu kufanya kila kitu peke yako, tumia fizikia ya neema kwa faida yako. Fizikia inahusika na jinsi vitu vianavyojongea na nguvu inayovifanya vijongee. Kwnye fizikia ya neema, Roho Mtakatifu ndiye Kocha wako- Atakupa mikakati bora, Neno la Mungu ni dira yako inayokupa mwelekeo; imani ndiyo baiskeli yako - ndio unayotumia kuelekea lengo lako, na malaika wako kwenye timu yako tayari kutumikia na kusaidia kwa njia yoyote unayohitaji. Kaa karibu na ujumbe wa neema; iweke mbele yako, na utajikuta unashinda kwa urahisi.

## UKIRI WA KINABII

**Kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo inathibitishia ushindi wangu katika kila uwanja. Nimefokasi kwenye mstari wa kumalizia, nimewekwa kwenye njia ambayo lazima niifuate. Kwa neema ya Mungu, ninawasukuma adui zangu na kukanyaga kikwazo chochote kinachonipinga. Neema isiyoweza kushindwa inafanya kazi ndani yangu, na kila kitu ninachohusishwa kinafanikiwa.**

**SOMO LA ZIADA:** Wafilipi 2:13



**Mhubiri 10:19**
**"Karamu hufanywa kwa ajili ya kicheko, Na divai huyafurahisha maisha; Na fedha huleta jawabu la mambo yote."**

Watu wengi huhudhuria makanisani ili kupata miujiza kuwa fedha inaweza kusuruhisha. Kwa kweli, asilimia tisini ya mahitaji ya maombi yangeweza kutoweka kama muhitaji angekuwa tu na fedha za kutosha. Biblia inasema kwamba pesa ni jawabu la mambo yote. Hiyo ina maana kila unapoona watu wakihangaika na kulumbana, ujue suala la pesa limewekwa mezani. Kila kitu kimefungwamanishwa kwenye pesa. Tatizo ni kwamba Wakristo wengi ambao wanahitaji fedha zaidi ni wale ambao wanazungumza vibaya zaidi kuhusu pesa. Wakristo wengi hawako huru kuzungumzia pesa kwa sababu walifundishwa kuwa pesa kwa asili ni mbaya. Sio kweli. Pesa ni za kiroho. Huchukua umbo la mmiliki wake na husikiliza mmiliki wake. Kwa mfano, pesa ya mtumia madawa ya kulevya zinakuwa pesa za madawa ya kulevya. Fedha za mwana mfanyabiashara mjuvi huwa uwekezaji ambao huzalisha pesa zaidi. Pesa za mtoaji hufanyika mbegu. Wakristo ndio watu wanaofuzu zaidi kuwa na pesa. Sisi ndio watunzaji walioteuliwa wa utajiri wa ulimwengu huu. Unatakiwa kuwa na pesa, wewe na vizazi vyako. Jifunze kuwa huru kuzungumza juu ya pesa kwa njia nzuri, haswa ikiwa unataka kuwa nazo zaidi. Jizoeze, na uendelee kuzungumza juu yake. Unapoendelea kuzungumza, pesa zitajibu.

## UKIRI WA KINABII

**Pesa haitakuwa shida kwangu. Nimeziteka pesa. Naweza kuzipata wakati wowote. Kunapokuwa hakuna fedha, naziumba. Pochi yangu ina pesa. Akaunti yangu ya benki ina pesa. Ninaziita pesa kwenye uhalisia. Pesa zinanijia kutoka kila mahali, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Mithali 13:22

# SCRIPTURE PASSAGE FOR PROTECTION

## ISAIAH 54:

14 I AM BUILD SOLID, GROUNDED IN RIGHTEOUSNESS,
FAR FROM ANY TROUBLE—NOTHING TO FEAR!
FAR FROM TERROR—IT WON'T EVEN COME CLOSE!

15 IF ANYONE ATTACKS ME,
I WILL NOT THINK FOR A MOMENT THAT GOD SENT THEM,
AND IF ANY SHOULD ATTACK ME,
NOTHING WILL COME OF IT.

16 GOD CREATED THE BLACKSMITH
WHO FIRES UP HIS FORGE
AND MAKES A WEAPON DESIGNED TO KILL.
HE ALSO CREATED THE DESTROYER—

17 BUT NO WEAPON THAT CAN HURT ME
HAS EVER BEEN FORGED.
ANYONE WHO ACCUSES ME
WILL BE DISMISSED AS A LIAR.
I AM GOD'S SERVANT SO THIS IS WHAT I CAN EXPECT
GOD WILL SEE TO IT THAT EVERYTHING
WORKS OUT FOR THE BEST FOR ME."

THIS IS WHAT GOD SAYS TO ME AND IT WILL NOT FAIL IN JESUS'S NAME!



# HAVE YOU RECEIVED JESUS CHRIST YET?

WE INVITE YOU TO MAKE JESUS CHRIST THE LORD OF YOUR LIFE BY PRAYING THIS PRAYER;

"O LORD GOD, I COME TO YOU IN THE NAME OF JESUS CHRIST. I BELIEVE WITH ALL MY HEART IN JESUS CHRIST, SON OF THE LIVING GOD. I BELIEVE HE DIED FOR ME AND GOD RAISED HIM FROM THE DEAD. I BELIEVE HE'S ALIVE TODAY. I CONFESS WITH MY MOUTH THAT JESUS CHRIST IS THE LORD OF MY LIFE FROM THIS DAY. THROUGH HIM AND IN HIS NAME, I HAVE ETERNAL LIFE; I'M BORN AGAIN. THANK YOU LORD, FOR SAVING MY SOUL! I'M NOW A CHILD OF GOD. HALLELUIAH!"

CONGRATULATIONS! YOU ARE NOW A CHILD OF GOD.

TO RECEIVE MORE INFORMATION ON HOW YOU CAN GROW AS A CHRISTIAN, PLEASE GET IN TOUCH WITH US ON

UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209

WWW.UEBERTANGEL.ORG | WWW.GOODNEWSWORLD.COM


TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209
www.goodnewsworld.com